TANGAZO LA SERIKALI NA. 232 la tarehe 4/4/2025

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 16(1))*

SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SINGIDA YA MWAKA 2025

Jina

TS Na. 221 la 2024

1.Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Manispaa ya Singida ya Mwaka 2025, na itasomwa kwa pamoja na Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Manispaa ya Singida ya Mwaka 2024 ambayo hapa imerejewa kama "Sheria Ndogo Kuu".

Marekebisho ya aya ya 6

2. Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa kwa kufuta na kuandika upya aya ya 6 kama ifuatavyo:

"Muda wa kukusanya ada na ushuru

6. Halmashauri itahakikisha kuwa ada au ushuru unakusanywa wakati wote katika maeneo yake."

Marekebisho ya Jedwali la Kwanza

3. Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa katika Jedwali la Kwanza-

(a) katika kipengele cha 6 cha Sehemu ya Tano kwa kuongeza neno "binafsi" baada ya neno "kampuni"; na

(b) katika Sehemu ya Kumi na Tisa kwa kuongeza vipengele vifuatavyo mara baada ya kipengele cha 7:

| Namba | Aina ya bidhaa | Gari ujazo (ukubwa wa tani) | Gharama za ushuru (Tsh) |
|---|---|---|---|
| 8. | Bidhaa | - | 1000.00/= |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | zilizobebwa kwenye bajaji | | |
| 9. | Bidhaa zilizobebwa kwenye pikipiki ya miguu miwili | - | 500.00/= |

(c) kwa kufuta Sehemu ya Ishirini; na

(d) kwa kubadili mpangilio wa Sehemu ya Ishirini na Moja hadi Sehemu ya Ishirini na Nane kuwa Sehemu ya Ishirini hadi Sehemu ya Ishirini na Saba mtawalia.

Dodoma
12 Machi, 2025

MOHAMED OMARY MCHENGERWA
*Waziri wa Nchi- Ofisi ya Rais,*
*Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa*